(96)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Bima,
S.L.P 845,
67128 MOROGORO
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Simu ya Bure: 113 au *113#
Barua pepe: rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

MOROGORO NOVEMBA, 2022

TAKUKURU YAZIDI KUWAFIKIA WANANCHI

Ndugu WanaHabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Septemba 2022 msisitizo uliwekwa katika kazi za UZUIAJI RUSHWA, ambapo pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, tumeweza kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi pamoja na watumishi wa umma na sekta binafsi, kupitia mikutano ya hadhara, semina na TAKUKURU Inayotembea. Kazi hii ilifanyika ili kuwahamasisha wananchi washiriki katika kutokomeza vitendo vya rushwa. Aidha katika elimu hiyo msisitizo ulitolewa katika uzingatiaji wa misingi ya maadili pamoja na utii wa sheria za nchi.

Ndugu WanaHabari

1. UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Kwa kuzingatia umuhimu wa miradi ya maendeleo kwa wananchi na kwamba Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imefuatilia utekelezaji wa **miradi ya maendeleo 26** yenye thamani ya **Shs. Bilioni 9.114** katika sekta za Elimu, Afya, Ujenzi, na Maji. Katika ufuatiliaji huo, **TAKUKURU ilibaini mapungufu yafuatayo:-**

- **Katika mradi wa utengenezaji wa viti na meza** katika shule ya sekondari Vidunda wenye thamani ya Shs. 12,000,000.00.
- Mapungufu yaliyobainishwa ni pamoja na baadhi ya viti kuwa vifupi, baadhi ya meza kutokuwa na droo za kuwekea madaftari na pia mbao zilizotumika zilikuwa chini ya kiwango.

- TAKUKURU iliagiza malipo ya kazi hiyo yasifanyike hadi kazi hiyo itakapofanyiwa marekebisho.
- **Katika mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Idunda – Ulanga** wenye thamani ya shs. 50,000,000.00 TAKUKURU imebaini kwamba Njia ya walemavu ilikuwa haijajengwa.
- Ili kutatua mapungufu hayo, TAKUKURU iliagiza Mkandarasi -kuitekeleza kazi hiyo mapema.

TAKUKURU inatoa rai kwa wasimamizi wote waliopewa dhamana ya kusimamia miradi hiyo wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na kuhakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika kwa wakati na thamani ya fedha iliyotolewa na kutumika inaonekana. Endapo kutakuwepo na ubadhirifu na ufujaji, TAKUKURU haitasita kuwachukulia hatua wahusika.

Ndugu WanaHabari

1.1 UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO 19

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2022, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imeweza kufuatilia jumla ya **miradi ya UVIKO 13 yenye thamani ya shs. Bilioni 2.9** katika sekta za Elimu, Afya na Maji. Katika Miradi hiyo hakuna kasoro ambazo ziliweza kubainika.

Ndugu WanaHabari

1.2 Uchambuzi wa Mifumo

Katika kipindi tajwa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imefanya chambuzi za mifumo **7** zinazohusiana na:-

- Mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kilosa.
- Mianya ya rushwa katika mapato na matumizi kijiji cha Msolwa Ujamaa Kilombero.
- Mianya ya rushwa katika utendaji kazi na usimamizi wa miradi ya maendeleo.
- Mianya ya rushwa katika uunganishaji wa umeme kwa wateja wilaya ya Malinyi.
- Mianya ya rushwa katika wa ujenzi wa miradi ya maendeleo Kata ya dakawa
- Mianya ya rushwa katika ujazaji wa leja za dawa na vifaa tiba katika Zahanati ya Ndugumi – Gairo
- Mianya ya rushwa katika uvunaji wa mazao ya misitu Wilaya ya Ulanga.

Kilichobainika kupitia chambuzi hizo na hatua zilizofuata ni kama ifuatavyo:-

S/N	UCHAMBUZI	KILICHOBAINIKA	HATUA ILIYOCHUKULIWA
1	Mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kilosa.	Wauguzi kuomba fedha kutoka kwa wagonjwa kwa ajili ya kuwanunulia dawa.	Wagonjwa kutowapatia fedha wauguzi kwa ajili ya kuwanunulia dawa badala yake wajinunulie wenyewe
2	Mianya ya rushwa katika mapato na matumizi – Msolwa Ujamaa	Fedha zilizokuwa zinakusanywa zilikuwa haziingizwi kwenye vitabu.	Maelekezo yalitolewa fedha zote zinazoingia ziingizwe kwenye vitabu
		Fedha zilikuwa zinatumika kabla ya kupelekwa benki	Wahusika walielekezwa kupeleka fedha benki kabla ya kuzitumia
3	Mianya ya rushwa katika wa ujenzi wa mradi wa Kituo cha Afya Kata ya Dakawa	Kutokuwa na ushirikiano wa wataalam kutoka Halmashauri na Kamati ya Ujenzi ya Kituo ha Afya Kata.	Maelekezo yalitolewa kwa wataalam kutoa ushirikiano kwa kamati za ujenzi
		Kutokuwapo kwa matumizi ya store ledger	Maelekezo yalitolewa store ledger ianze kutumika
		Kamati za ujenzi kutokuwa na uelewa kuhusiana na majukumu yao	Kamati za ujenzi zielimishwe kuhusiana na majukumu yao.
4	Mianya ya rushwa katika ujazaji wa leja za dawa na vifaa tiba katika Zahanati ya Ndugumi – Gairo	Kulikuwa na tatizo kubwa la wizi kufuatia dawa na vifaa tiba kutoingizwa katika leja za dawa	Maelekezo ya kuanza kutumia leja za dawa zote zinazonuliwa na kupelekwa katika zahanati hiyo.
5	Mianya ya rushwa katika utendaji kazi na usimamizi wa miradi ya maendeleo	Usimamizi mbovu wa miradi ya maendeleo.	Wataalam wakague miradi kwa wakati na kwa weledi
6	Mianya ya rushwa katika uunganishaji	Wateja wa REA walikuwa wakiombwa rushwa kama	Elimu ilitolewa kwa wateja ili watoe taarifa kwa

	wa umeme kwa wateja wilaya ya Malinyi.	sharti la kuwaunganishia umeme.	TAKUKURU pale wanapoombwa rushwa.

Vikao/warsha:

Warsha mbili **(2)** kuhusu Mfumo wa mapato na matumizi katika Kijiji cha Msolwa Ujamaa pamoja na Mianya ya rushwa katika ujenzi wa mradi wa Kituo cha Afya Kata ya Dakawa ilifanyika kwa lengo la kuweka maazimio ya kuziba mianya ya rushwa.

Katika kikao kuhusiana na **Mfumo wa Mapato na Matumizi** katika Kijiji cha Msolwa Ujamaa, wajumbe waliweka maazimio ya kuingiza fedha zote katika vitabu na kutotumia fedha hizo kabla hazijaingizwa Benki.

Aidha katika Kikao cha wadau kuhusu **ujenzi wa mradi wa Kituo cha Afya** Kata ya Dakawa wajumbe waliweka maazimio ya wataalam kushirikiana kikamilifu na wajumbe wa Kamati za ujenzi na pia matumizi ya leja ya vifaa kuzingatiwa.

Ndugu WanaHabari

1. 4 MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2022

Mwenge wa Uhuru 2022 ulikimbizwa Mkoani Morogoro mwezi Agosti 2022. Wakati wa mbio hizo, Mwenge wa Uhuru 2022 uliweza kutembelea, kukagua na kuzindua jumla ya **miradi 41** katika sekta za Afya, Elimu, Maji, Ujenzi, miradi ya vijana na miradi ya watu binafsi ikiwa na thamani ya **shs. Bilioni 13.**

Wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2022 **miradi mitatu** ya Sekta ya Afya ambayo ni pamoja na mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya Itete - Malinyi wenye thamani ya shs. 345,280,000.00 ulikataliwa, mradi wa Kituo cha Afya Igima - Kilombero wenye thamani ya shs. 500,000.00 na Mradi wa jengo la wagonjwa wa dharura Hospitali ya Wilaya ya Gairo wenye thamani ya shs. 300,000,000.00 iliwekewa mawe ya msingi kwa maelekezo kutoka kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge ya kufanya uchunguzi ili kubaini thamani ya fedha ya miradi hiyo.
Uchunguzi wa miradi hiyo unafanyika na uko katika hatua mbalimbali.

2. UELIMISHAJI UMMA

Katika kipindi husika, elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi pamoja na watumishi wa umma na sekta binafsi, ilitolewa kwa njia mbalimbali kama zilivyoainishwa hapa chini:

NA.	KAZI ILIYOFANYIKA	UFAFANUZI
1.	Kutembelea na kuziimarisha klabu za wapinga rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo.	Klabu za wapinga rushwa 297 zilifikiwa kwa lengo la kuwaelimisha wanafunzi kama njia ya kuwajengea uzalendo na ujasiri wa kufichua vitendo vya rushwa ikiwemo rushwa ya ngono.
2.	Kutoa Semina kwa watumishi wa Umma, Sekta binafsi na wananchi.	Makundi mbalimbali yalijengewa uwezo kupitia semina 46 zilizotolewa kwa lengo la kudhibiti rushwa. Makundi yaliyofikiwa ni pamoja na makarani wa sensa, wasimamizi wa mahudhui na tehama mwaka 2022, Taasisi ya Elimu Tanzania, Wakala wa Huduma za Misitu, Watumishi wa mfuko wa hifadhi ya taifa ya jamii, Jeshi la Akiba, Mamlaka ya masoko ya mtaji na dhamana, Wakala wa mbegu za kilimo, wasimamizi wa Mitihani ya darasa la saba mwaka 2022.
3.	Kuelimisha wananchi kupitia mikutano ya Hadhara	Jumla ya mikutano ya hadhara 60 ilifanyika katika maeneo ya vijiji pamoja na mitaa kwa lengo la kuwajengea wananchi uelewa ili waweze kushiriki katika ufuatiliaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kudhibiti vitendo vya rushwa.
4	TAKUKURU inayotembea	**Tarehe 22.07.2022** TAKUKURU ilifanya Mikutano katika vijiji vya **Kiwege** na **Ngerengere** Kata ya Ngerengere kupitia **TAKUKURU inayotembea** kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi kuhusiana na utendaji kazi wa Kituo cha Afya Ngerengere ambapo wananchi walifikisha malalamiko yao kuhusiana akina mama wajawazito kuombwa rushwa na watumishi wa Kituo hicho kama sharti la kuwahudumia wakati wa kujifungua. Kupitia mikutano hiyo hakuna mwananchi aliyethibitisha tuhuma hiyo, na kupitia mikutano hiyo, Mganga mfawidhi wa Kituo cha Afya Ngerengere aliwasihi wananchi kujinunulia vifaa wenyewe pale ambapo vifaa havipo na wasiwapatie fedha watumishi wa kituo hicho kwa ajili ya kwenda kuwanunulia.
4.	Taarifa kwa Umma kupitia vyombo vya	Kupitia vyombo vya habari, Wananchi walifahamisha kuhusu utendaji kazi wa TAKUKURU hususani hatua

	habari- 2	mbalimbali zilizochukuliwa katika udhibiti wa vitendo vya rushwa.
5.	Uandishi wa Makala/ Habari	Utolewaji wa habari mbalimbali kuhusu mafanikio ya mapambano dhidi ya rushwa

Ndugu wanaHabari

3. UCHUNGUZI NA MASHTAKA:

Pamoja na kuwashirikisha wananchi katika udhibiti wa rushwa, bado vitendo vya rushwa vinaendelea kujitokeza katika jamii. Hivyo kwa kipindi tajwa tumepokea jumla ya malalamiko **106** na kati ya hayo, malalamiko **53** yanahusiana na vitendo vya rushwa na uchunguzi wake uko katika hatua mbalimbali. Malalamiko **53** yasiyohusu rushwa watoa taarifa walishauriwa jinsi ya kufuatilia malalamiko yao pamoja na kuwatatulia kero zao kwa kuwapeleka kwenye mamlaka husika.

Sekta zilizolalamikiwa ni kama ifuatavyo:-

Serikali za Mitaa/ Vijiji na Kata **(27),** TAMISEMI **(13),** Vyama vya Siasa **(9),** Polisi **(8),** Elimu **(8),** Mahakama **(6),** Ardhi **(6),** Taasisi za Fedha **(5),** Ujenzi **(4),** Vyama vya Ushirika na Vicoba **(4),** Afya **(3),** Maliasili **(3),** Maji **(2),** Takwimu na Sensa **(2),** Sekta Binafsi **(2),** Kilimo **(1),** Usafirishaji **(1),** Mifuko ya Hifadhi ya Jamii **(1) na** Maendeleo ya Jamii **(1).**

Pia, jumla ya **kesi mpya (03)** zimefunguliwa na kufanya jumla ya **kesi 17** zinazoendelea mahakamani. Katika kipindi husika TAKUKURU ilishinda Kesi mbili (02).

Tunatoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU na pia wawe na utayari wa kutoa ushahidi Mahakamani pindi watakapohitajika ili Mahakama iweze kutenda haki na kutoa hukumu stahili kwa wale wanaotuhumiwa kwa kutenda makosa.

4. MIKAKATI YA OKTOBA – DESEMBA 2022

Kwanza, Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika miradi inayotekelezwa Mkoani Morogoro kwa kushirikiana na taasisi zilizopewa jukumu la kutekeleza miradi hiyo ambazo ni pamoja na TARURA, RUWASA, TANROAD, MORUWASA Halmashauri n.k. Ili kufanikisha mkakati huo, TAKUKURU imefanya mawasiliano na Meneja wa TARURA na RUWASA ambao wameafiki kufanya ukaguzi wa miradi kwa kushirikiana. Aidha mawasiliano yatafanyika kwa Taasisi zilizobaki.

Pili, Tutafuatilia kwa ukaribu fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na mabweni kwa ajili ya wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza mwaka 2023.

Niwakumbushe wasimamizi wa miradi hiyo waweze kutekeleza kwa haraka kama maagizo yalivyotolewa ili ifikapo mwezi Januari 2023, wanafunzi wa kidato cha kwanza waweze kuanza masomo yao.

Tatu, tunaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa jamii kupitia mpango wa **TAKUKURU INAYOTEMBEA**, pamoja na mikutano ya hadhara. Lengo ni kuwafikia wananchi zaidi ili waweze kushirikiana na TAKUKURU katika kudhibiti vitendo vya rushwa.

Tunawasihi viongozi wa Mitaa na Vijiji kuiga mfano wa **Mwenyekiti wa Mtaa wa Saadan Kata ya Mwembesongo** kwa kutoa mialiko kwa TAKUKURU pale wanapokuwa na Mikutano yao, ili waweze kupatiwa elimu kuhusiana na rushwa.

Vilevile tutaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi katika Klabu za Wapinga Rushwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo ili kuwajengea uwezo wanafunzi hao kukataa kujihusisha katika vitendo vya rushwa. Pia tutaendelea kutoa elimu kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kupitia semina ili waweze kutekeleza wajibu wao kwa uadilifu na uaminifu.

Nne, Tutaendelea kufuatilia kwa ukaribu mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika halmashauri ili kudhibiti upotevu wa fedha za umma.

Tano, Tutaendelea kufuatilia matumizi ya mbolea ya ruzuku zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya wakulima. Aidha nitoe rai kwa wote watakaojihusisha na udanganyifu wowote kwa ajili ya kuhujumu mbolea ya ruzuku, watachukuliwa hatua kali.

Mwisho, tunawasihi wananchi waendelee kushirikiana na TAKUKURU katika kupambana na vitendo vya rushwa na pia wawe jasiri, wazalendo na wenye utayari wa kutoa ushahidi Mahakamani pale wanapohitajika ili haki iweze kutendeka kwa wanaotuhumiwa na makosa ya rushwa.

Manyama Tungaraza,
Mkuu wa TAKUKURU (M), Morogoro
Simu ya Mkononi: 0738 150 143